**JARIDA LA ACT**
**TOLEO NA.44 (Julai - Desemba 2022)**
**Tunaunganisha, Shawishi na Kutetea**

## *Wajumbe wa Bodi*

Dkt. Jacqueline Mkindi

**Mwenyekiti**

Mhe. Jitu Soni- Makamu/Mkt

Dkt. Sinare Y. Sinare - Mjumbe

Bw. Fabian Mwakatuma - Mjumbe

Bw. Enock Ndodole - Mjumbe

Bw. Zubery Mwachulla- Mjumbe

Bw. Omary Mwaimu - Mjumbe

Bw. Joeseph Masimba - Mjumbe

Bibi. Elde Kimaro - Mjumbe

Bw. Abel Lyimo – Mjumbe

## *Yaliyomo*

ACT Yashiriki Maonesho ya Nane Nane

Kikao cha Kumi cha Kamati ya Kitaifa

Mafunzo kwa Wakulima wa Mvomero

Ziara ya Mafunzo Ujerumani

Warsha ya Kikanda

Wakulima Wajadiliana na Wafanyabiashara

Mkutano wa Kimataifa wa Wakulima Vijana

Programu ya Ustawi wa Biashara ya Kilimo

Maonesho ya Kilimo

Siku ya Sekta Binafsi

## Waziri Mkuu, Akizindua Programu ya Vijana- kwenye Kilimo



## TUKIO LIJALO

Maonesho ya Kimataifa ya mboga mboga na matunda **(FRUIT LOGISTICA**)– Messes, Berlin **Feb 8-10, 2023**

(Kwa taarifa zaidi, wasiliana na TAHA kupitia **+255 763 718 849**)

# ACT YASHIRIKI NANE NANE KITAIFA- MBEYA

Maonesho ya Kitaifa ya Kilimo maarufu kama Nane Nane hufanyika kwa wiki moja (kuanzia tarehe 1 hadi 8 Agosti), ni tukio la kila mwaka ambalo hutoa fursa ya kuonesha bidhaa zitokanazo na kilimo, vumbuzi na teknolojia mpya kwa maendeleo ya kilimo, na mbinu bora zitakazosaidia kuboresha sekta ya kilimo. Maonesho hayo, huwaleta karibu wakulima, wafanyabiashara, vyama vya wakulima, vyama vya ushirika, taasisi za fedha, Serikali na taasisi zake kwa lengo la kusherehekea na kutambua michango yao katika kukuza na kuchochea uchumi wa taifa. Maonesho ya Kilimo hufanyika katika kanda saba nchini kote yaani; Kanda ya Mashariki (Morogoro), Kanda ya Kaskazini (Arusha), Kanda ya Magharibi (Tabora), Kanda ya Kusini (Lindi), Kanda ya Kati (Dodoma), Kanda ya Nyanda za Juu Kusini (Mbeya), na Kanda ya Ziwa (Mwanza). Maonesho ya Mwaka huu yalipambwa na kaulimbiu isemayo *"Ajenda 10/30: Kilimo ni Biashara: Shiriki Kuhesabiwa kwa Mipango Bora ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi"*. Ngazi ya kitaifa maonesho yalifanyika katika viwanja vya John Mwakangale Mkoani Mbeya na kufunguliwa rasmi na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Philip I. Mpango. Katika hotuba yake, Makamu wa Rais alizitaka benki za ndani kutoa fursa zaidi za mikopa kwa wakulima, wavuvi, na wafugaji ili kuongeza uwekezaji na tija katika jitihada za kukabiliana na changamoto ya ukosefu wa ajira nchini.

Tarehe 3 Agosti, Waziri Mkuu Mhe. Kassim M. Kassim alizindua Programu ya Ajira kwa Vijana kupitia Sekta ya Kilimo *"Building a Better Tomorrow-Youth Initiative for Agribusiness (BBT-YIA)"* inayolenga kuongeza ushiriki wa vijana katika kilimo kwa kuwapatia mafunzo, mashamba, mitaji na kuwaunganisha na fursa za masoko. Mpango huo ulizinduliwa sambamba na Kliniki ya Wakulima "Farm Clinic", programu ya ubia baina ya Serikali, Mwananchi Communications Limited, na Vodacom Tanzania. Kliniki hiyo, itasaidia kutambua idadi ya wakulima nchini kupitia mifumo rasmi ya usajili. Ubia huu, utaisaidia Serikali kutambua na kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili wakulima nchini.




***Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akizindua Programu ya Vijana kwenye Kilimo jijini Mbeya. Kulia ni Spika wa Bunge Dkt. Tulia Ackson. Wengine ni Naibu Waziri wa Kilimo Anthony Mavunde (kushoto) na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya Juma Homera***

ACT ilishiriki Nane Nane ngazi ya Kitaifa, sambamba na wadua wengine kwenye banda la ***"SAGCOT SQUARE***". ACT ilishiriki sherehe hizo, kwa lengo la kuonesha mchango wake katika kutetea uwepo mazingira wezeshi ya kilimo biashara, na kutoa fursa kwa wakulima kutoka Mkindo na Dakawa kukutana na wadau kama vile YARA, Raphael Group Limited (RGL) kwa lengo la kuboresha shughuli zao za kiuchumi. Banda la ACT lilitembelewa na wageni kwa lengo la kufahamu kazi zake, mabadiliko ya kisera, teknolojia za kilimo, na kuboresha mahusiano ya kibiashara na wakulima kutoka Mkindo na Dakawa.




**Mkurugenzi Mtendaji wa Baraza la Kilimo Tanzania (katikati) akiwa na wanufaika wa Mradi wa FO4ACP kwenye maonesho ya kilimo Mbeya.**




Akizungumza kwenye kilele cha maonesho ya Nane Nane Mbeya, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia H. Suluhu alisema kuwa "***Tayari tumejadiliana na benki za ndani kuona namna gani wanaweza kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa vijana"*** Aliongezea kuhusiana na soko, Rais Dkt. Samia aliwahakikishia vijana kuwa Serikali imepata soko la uhakika nje ya nchi na imejipanga vyema kuweka mazingira wezeshi ya kuzalisha kibiashara. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alizindua mpango wa ruzuku utakaowawezesha wakulima kupata mbolea kwa bei nafuu kwa msimu wa kilimo 2022/23. Mpango huo unaratibiwa na Wizara ya Kilimo kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) na ulianza Agosti 15 mwaka huu.

# MKUTANO WA KUMI WA KAMATI YA KITAIFA

Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara iliandaa Mkutano wa kumi (10) wa Kamati ya Kitaifa inayoshughulikia Viwango vya Afya ya Mimea, Wanyama na Usalama wa Chakula (National Sanitary and Phytosanitary Measures Committee - NSPSC). Mkutano huo ulifanyika kuanzia tarehe 10 hadi 12 Agosti 2022 katika Hoteli Nashera, Mkoani Morogoro na uliandaliwa kwa ufadhili wa Shirika la Trademark East Africa (TMEA). Kikao kiliongozwa na Bw. Ombeni N. Mwasha (Mkurugenzi wa Kitengo cha Mtangamano wa Biashara) kutoka Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara akisaidiwa na Bw. Lazaro Msasalaga (Mkurugenzi wa Udhibiti Ubora Shirika la Viwango). (TBS); lengo kuu la Mkutano huo, ilikuwa ni kujadili utekelezaji wa shughuli za Kamati ya Kitaifa ya kushughulikia Vigezo vya Afya ya Mimea, Wanyama na Usalama wa Chakula. ACT iliwakilishwa na Bw. Khalid Ngassa, Meneja Huduma na Maendeleo ya Uanachama ambaye alitoa wasilisho la utekelezaji wa shughuli zilizotekelezwa na ACT zinazohusiana na afya ya Mimea, Wanyama na Usalama wa Chakula kwa kipindi cha miezi sita. TMEA inatekeleza mradi wa miaka mitatu nchini, ambao umeanza Julai 2021 mpaka Julai 2024, na umelenga zaidi Afya ya Mimea, Wanyama na Usalama wa Chakula.

TMEA ilianzishwa mwaka 2010 ili kukuza ustawi wa biashara ukanda wa Afrika Mashariki. TMEA inafanya kazi kwa karibu na mashirika ya kikanda ya kiserikali, ikiwa ni pamoja na Umoja wa Afrika (AU), Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Mamlaka ya Maendeleo ya Kiserikali (IGAD), Soko la Pamoja la Afrika Mashariki na Kusini (COMESA), Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC), serikali za kitaifa, sekta binafsi, na mashirika ya kiraia.


WAJUMBE WA MKUTANO WA KUMI(10) WA KAMATI YA KITAIFA
INAYOSHUGULIKIA VIWANGO VYA AFYA YA MIMEA,
WANYAMA NA USALAMA WA CHAKULA.(SPS)
10-12 AGOSTI 2022
NASHERA HOTEL
MOROGORO

# MAFUNZO YA MBINU ZA KILIMO MVOMERO

Oktoba 24 hadi 27 2022, Maafisa Mradi kutoka ACT Bw. Obedi Abraham na Bi. Agnes Ngondo waliendesha mafunzo ya siku nne kuhusu “*Mabadiliko ya Tabianchi, Mseto wa mazao na kilimo shadidi kwenye zao la mpunga (SRI)*” kwa wakulima wa Wilaya ya Mvomero-Mkoani Morogoro katika skimu za umwagiliaji,- Mkindo na Dakawa. Mafunzo yalilenga kuwajengea uwezo wakulima kwa kuwapa mbinu bora za kilimo hasa kilimo shadidi ambacho kwa kiasi kikubwa hakitegemei mvua, na mbinu bora za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Washiriki 34 walipata mafunzo hayo ikijumuisha maafisa ugani, wakulima viongozi, wauzaji wa pembejeo n.k. Mradi wa SFOAP ni wa miaka mitano (2019-2023) unafadhiliwa na Shirikisho la Wakulma Kusini mwa Afrika (SACAU) na ulilenga kuwafikia wakulima wadogo wapatao 16,000 wakiwemo wanawake na vijana katika Wilaya ya Mvomero kwa kuwapa mafunzo ya kilimo shadidi na hifadhi. Mradi umefanikiwa kuwafikia wakulima wadogo 19,000 kutoka Mkindo na Dakawa, inakadiriwa mpaka 2023 wakulima 24000 watanufaika na mradi.



***Washiriki wakiwa kwenye picha ya pamoja na wa kufunzi***

# ZIARA YA MAFUNZO, UJERUMANI

Andreas Hermes Akademie (AHA International) kwa kushirikiana na Shirikisho la Wakulima Kusini mwa Afrika (SACAU) waliandaa ziara ya mafunzo ya wiki moja Ujerumani Mashariki (Bernburg City) kuanzia tarehe 8 hadi 15 Oktoba 2022 kwa nchi wanachama wa SACAU (Malawi, Lesotho, Zimbabwe, Madagascar, Mauritius, Msumbiji, Seychelles, Namibia, E-swatin, Tanzania, na Afrika Kusini). Ziara hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa mradi, unaolenga kuimarisha uwezo wa wanachama wake katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kubadilishana uzoefu; AgriKontakte International iliratibu ziara hiyo, kwa kuandaa semina na vikao vya kubadilishana uzoefu/kujifunza kuhusu mabadiliko ya tabianchi. ACT iliwakilishwa na Bw. Obed Abraham na Bi. Avelina Bernard, Maafisa Miradi kutoka ACT walipata fursa ya kutembelea Chuo Kikuu cha Gottingen, Taasisi ya Utafiti wa Athari za Hali ya Hewa (Potsdam Institute for Climate Impact Research- PIK), na kituo cha kilimo cha Augustenberg kama sehemu ya kujifunza. Ziara ya mafunzo Ujerumani, ilikuwa na manufaa makubwa; washiriki walipata uzoefu wa vitendo kutoka kwa wataalamu na wakulima kuhusu mabadiliko ya tabia nchi. Kwa kifupi; Nchi za SADC zinapaswa kuandaa mikakati inayohusiana na ustahimilivu wa hali ya hewa inayoendana na jiografia ya sehemu husika, na kuwekeza kwenye teknolojia  za hali ya hewa (dijitali).




***Washiriki wakiwa kwenye picha ya pamoja baada ya kutembela shamba lililopo mji wa Bernburg, Saxony-Anhalt,***

# EABC YAFANYA MKUTANO WA KIKANDA

Baraza la Biashara la Afrika Mashariki (EABC) kwa kushirikiana na TradeMark East Africa (TMEA) waliandaa mkutano wa kikanda uliokutanisha wadau kutoka Sekta Binafsi na Umma kujadili utekelezaji wa makubaliano ya Viwango vya Afya ya Mimea, Wanyama na Usalama wa Chakula (SPS) katika Nchi za Afrika Mashariki (EAC). Mkutano huo, ulifanyika Oktoba 26 na 27 2022, katika Hoteli ya Panari- Nairobi Kenya. Mkutano ulijikita katika kujadili maboresha ya utekelezaji wa Viwango vya Afya ya Mimea, Wanyama na Usalama wa Chakula ngazi ya kikanda sambamba na kupitia muundo, sera na changamoto za utekelezaji wake.

Warsha ilikuwa na malengo yafuatayo;

1. Kuhamasisha Sekta ya umma na Binafsi kutekeleza itifaki ya SPS ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki,
2. Kuboresha matumizi ya mfumo wa SPS ngazi ya kanda, na
3. Kuainisha mahitaji, mapungufu, na changamoto zinazokabili jumuiya ya wafanyabiashara; kuandaa mkakati kuzitatua kwa kuzingatia Itifaki ya SPS ndani ya ukanda wa Afrika Mashariki.

Warsha ilikutanisha washiriki kutoka nchi wanachama (Burundi, Kenya Rwanda, Sudan Kusini na Tanzania) wanaowakilisha; Vyama vya wazalishaji wa bidhaa; Mashirika ya Kitaifa ya Sekta binafsi; Wizara ya Kilimo, Mifugo na Ushirika, Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mashirika ya Viwango, Chemba za Biashara, Shirikisho la Wakulima Afrika Mashariki (EAFF), Vyama vya Wazalishaji wa Kuku, wanachama wa EABC, Chemba ya Wanawake Wafanyabiashara (TWCC), Watoa huduma katika tathmini za usalama na ulinganifu wa chakula na Vyombo vya habari. Kwa ufupi, washiriki walitoa michango yao katika utekelezaji wa itifaki ya SPS ngazi ya kanda kwa kuzingatia masuala yafuatayo;

1. Kuhuisha viwango vya bidhaa katika ngazi za kikanda na kitaifa kama vile ubora wa nafaka; teknolojia; chakula cha mifugo; na malisho ya wadudu,
2. Kutoa huduma kwa wadau wa mnyororo wa thamani kwa mfano mashine za kuondoa sumu kuvu; huduma za cheti cha ghala; kuwajengea uwezo wakulima juu ya mbinu bora za kuzuia upotevu wa mazao

baada ya mavuno; kuandaa matukio ya mwaka kama vile Maonesho ya Mwaka ya kuku nchini Tanzania; na kutoa taarifa sahihi  za wazalishaji,

3. Kuimarisha uwezo wa wadau katika kutekeleza matakwa ya kibiashara; kwa mfano kupima nafaka; mafunzo kwa wapimaji; uhamasishaji wa biashara zisizo rasmi mipakani; na kuwapa wakulima mashine za kubaini sumu kuvu kwenye nafaka.

Baraza la Kilimo Tanzania (ACT) liliwakilishwa na Mkurugenzi wa Sera, Mipango na Utetezi, Bi. Laetitia William ambaye alielezea uzoefu wake juu ya utekelezaji wa hatua zaViwango vya Afya ya Mimea, Wanyama na Usalama wa Chakula (SPS) nchini.




***Picha ya pamoja ya Washiriki wakati wa Mkutano Kikanda, Nairobi- Mkenya***

# WAKULIMA WAJADILI NA WAFANYABIASHARA

Oktoba 28 na 29 2022, ACT iliendesha warsha ya siku mbili iliyohusu "*Mahusiano ya kibiashara*" kwa wakulima wa wilaya ya Mvomero, Mkoani Morogoro kutoka skimu umwagiliaji za Mkindo na Dakawa. Warsha hiyo ililenga kuboresha mahusiano ya kibiashara baina ya wasindikaji na wakulima wadogo. Washiriki 96 walihudhuria wakiwemo wakulima vinara, wafanyabiashara, wasindikaji, na maafisa ugani. Kupitia warsha hiyo, washiriki waliweza kujadilia kwa kina masuala yanayohusiana na bei, taratibu za malipo, masharti ya bidhaa na masuala ambayo yanaweza kuchochea mazingira ya biashara yenye faida. Warsha hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa mradi wa FO4ACP (2019-2023) unaofadhiliwa na Shirikisho la Wakulima Kusini mwa Afrika (SACAU) unaolengo kuongeza pato la mkulima. Warsha iliendeshwa na  Bw. Obed Abraham, Bi. Agnes Ngodo kutoka Sekretarieti ya ACT, na Bw. Hoziel Foya - mwakilishi wa ACT Mvomero.

.




***Meneja mauzo kutoka Murzah Wilmar, Bw. Nuruel akiongea na wakulima kuhusu soko la bidhaa za kilimo, Mkindo***

# MKUTANO WA KIMATAIFA WA WAKULIMA VIJANA

Shirika la Pan African Farmers Organization (PAFO), kwa kushirikiana na washirika wake, waliandaa Mkutano wa Kimataifa wa Wakulima Vijana ambao ulifanyika Oktoba 24 hadi 29 2022 katika Hoteli ya Lemigo-Kigali Rwanda. Mkutano huo, ulipambwa na kaulimbiu isemayo *"Vijana kwenye maendeleo ya Kilimo na Ubunifu"***.** Mkutano huo, uliwakutanisha wawakilishi wawakulima vijana kutoka mabara matano ili kubadilishana uzoefu, kujadili changamoto na kupendekeza suluhu ya changamoto hizo. Mkutano huo, ulienda sambamba na uzinduzi wa *Mkakati wa Vijana na Kilimo Biashara*, chini ya Umoja wa Afrika (AU) unaolenga kuwezesha vijana wajasiriamali kushiriki katika kuandaa sera, kupitia na kufanya maamuzi kwa maslahi ya kuendeleza ustawi wa kilimo-biashara.




***Bw. Omary Mwaimu akiwa kwenye mkutano wa kimataifa wa vijana Kigali -Rwanda***

Bw. Omary Mwaimu, mjumbe wa Bodi ya ACT na Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya AMSHA ni miongoni mwavijana waliopata nafasi ya kushiriki mkutano huo. Bw. Mwaimu alitoa mtazamo wake juu ya mambo yanayokatisha tamaa ushiriki wa vijana katika sekta ya kilimo kama vile; mtazamo wa vijana na kilimo (mindset), ujuzi na maarifa ya biashara husika (agripreneurship skills). Bw. Mwaimu alielezea, mpango wa majaribio wakuwajengea vijana uwezo katika masuala ya kilimo biashara; unaotolewa kwa muda wa miezi 10, chini ya uratibu wa Shirika la Chakula Duniani (F.A.O Tanzania). Taasisi ya AMSHA na Halmashauri za miji (Rufiji, Kibiti, na Mkuranga) wanashirikiana kutoa mafunzo hayo na vijana 30 wameshanufaika na programu hiyo.

# PROGRAMU YA USTAWI WA BIASHARA YA KILIMO

Tarehe 3 Novemba 2022, Aceli Africa na Baraza la Kilimo Tanzania waliendesha warsha ya ufunguzi wa mafunzo ya kuwajengea uwezo wajasiriamali kwenye kilimo yaliyofanyika katika Hoteli ya Sea Cliff-Dar es Salaam. Programu ya Ustawi wa Biashara ya Kilimo itanufaisha wajasiriamali takribani 30, kwa kuwaongezea ujuzi na maarifa yanayohitajika katika kusimamia na kupanua wigo wa biashara zao sambamba na kuwaunganisha na taasisi za fedha kwa lengo la kupata mitaji ya kuendesha biashara zao. Taasisi ya African Management Institute (AMI), WYLDE International kutoka Kenya na TAPBDS ya Tanzania waliendesha ufunguzi wa mafunzo hayo. AMI itatoa mafunzo kwa wajasiriamali, huku WYLDE International na TAPBDS zitakuwa na jukumu la kushauri na kutoa miongozo ya kibiashara (mentorship). Baraza la Kilimo Tanzania liliwakilishwa na Bw. Khalid Ngassa - Meneja Huduma na Maendeleo ya Uanachama, katika hotuba yake alisisitiza washiriki kutumia mafunzo hayo kupata ujuzi utakaosaidia kukuza biashara na kuangalia masoko mapya ya bidhaa. Awamu ya pili na tatu ya maombi yatafunguliwa Januari 2023, wajasiriamali 60 wanatarajiwa kunafaika na programu.



***Picha ya pamoja ya washiriki wakati wa ufunguzi wa mafunzo kwa wajasiriamali kwenye kilimo, Dar es Salaam***

## MAONESHO YA KILIMO YA AFRIKA MASHARIKI

Agro-Food East Africa na Food-Pack Tech Tanzania waliandaa Maonesho ya Kilimo ya Afrika Mashariki yajulikanayo kama “***AgriTech East Africa EExhibition”*** yaliyofanyika kwa siku tatu kuanzia Novemba 21 hadi 23 katika Ukumbi wa Diamond Jubilee - Dar es Salaam. Maonesho hayo, yalikutanisha makampuni ya kimataifa ya kilimo, chakula, wataalamu wa teknolojia za chakula, watoa huduma za usindikaji na ufungashaji kutoka mataifa mbalimbali kwa lengo la kuonyesha teknolojia mpya za kilimo na vumbuzi, mbinu bora za kilimo au mbadala wa kukabiliana na changamoto zinazoikabili sekta ya kilimo. Maonesho ya mwaka huu, yalifunguliwa na Dkt. Stephen E. Ngailo-Mkurugenzi Mtendaji (Tanzania Fertilizer Regulatory Authority). Katika hotuba yake ya ufunguzi, alisisitiza makampuni ya kimataifa kuwekeza katika teknolojia ambayo inalenga kuendeleza sekta ya kilimo. Waonyeshaji wapatao 700 na wageni 1000 walihudhuria kutoka mataifa yafuatayo: India, Urusi, Misri, Uturuki, Hispania, Nigeria, Afrika Kusini, Uingereza, Italia, na Jumuiya ya Afrika Mashariki (Tanzania, Kenya na Uganda)..




***Picha ya pamoja: Watumishi wa ACT , na wakulima kutoka Mvomero wakati wa Maonesho ya Kilomo ya Afrika Mashariki, Dar es Salaam***

Maonesho yaliandaliwa chini ya Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) kwa kushirikiana na Baraza la Kilimo Tanzania (ACT), Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Chemba ya Wafanyabiashara wenye Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA), Chama cha Wafanyabiashara Wanawake Tanzania (TWCC), Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania (CTI) na Baraza la Mchele Tanzania (RCT). Miongoni mwa matunda ya maonesho hayo ni, kupatikana kwa mikataba ya kibiashara na masoko mapya ya bidhaa za kilimo.

# SIKU YA SEKTA YA BINAFSI NCHINI

Tarehe 2 Desemba 2022, Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) pamoja na washirika wake waliandaa Siku ya Kitaifa ya Sekta Binafsi iliyofanyika katika ukumbi  wa Superdome, Masaki - Dar es Salaam; Siku hiyo maalumu ililenga kujadili mafanikio na changamoto ya mazingira ya biashara nchini. Siku ya Sekta Binafsi ilipambwa na kaulimbiu isemayo ***"Kuongeza Ushindani wa Sekta Binafsi***". Hafla hiyo ilizinduliwa  na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dk.Philip I. Mpango, katika hotuba yake; Makamu wa Rais Mpango alielezea mwenendo wa utekelezaji wa mazingira ya biashara (Blue print for regulatory framework); mpnago huo wa kuwezesha mazingira ya kibiashara ulitolewa na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji mwezi Aprili 2018. Dk Mpango alisema utekelezaji wa Mpango huo ulioanza Julai 2019, umefikia asilimia 13 tu ya utekelezaji wake, na kumuagiza Dk. Kijaji kuhakikisha kufikia angalau asilimia 50 ya utekelezaji ifikapo mwishoni mwa mwaka ujao. Pia alisisitiza kuwa ushirikishwaji wa sekta binafsi katika Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPPs) haukuwa mzuri, aliiagiza Wizara ya Fedha na Mipango kushughulikia kwa haraka masuala yanayokwamisha ushiriki wa sekta binafsi. Usiku wa Sekta binafsi, ulipambwa na tuzo zilizotolewa kwa mashirika ya sekta binafsi vinara katika masuala ya Mazingira endelevu, Taasisi bora kwenye masuala ya Kijamii, na Biashara bora Bunifu. ACT iliibuka kinara katika kundi la taaisisi zilizofanya vizuri  katika kuchochea ongezeko la bajeti ya kilimo.




*Mwenyekiti wa ACT , Dkt. Jacqueline Mkindi (katikati)  na watumishi wa ACT kwenye usiku wa Sekta Binafsi Nchini, Dar es Salaam*




*Makamu wa Raisi wa Tanzania katika Siku ya Sekta Binafsi Tanzania 2022*

## Dira na Dhamira

**DIRA**

Kuwa na sekta ya kilimo iliofanikiwa, endelevu na shindani inayohakikisha usalama wa chakula na lishe unaotokana na msukumo wa kisekta binafsi.

**DHAMIRA**

Kutetea, kuratibu na kuwezesha mazingira rafiki kwa kilimo-biashara.

## Malengo ya ACT

- Kujenga mazingira wezeshi kwa kilimo-biashara
- Kujengea uwezo wanachama wa ACT katika utoaji wa huduma
- Kutuma na kupokea taarifa kutoka kwa wanachama na wadau wengine zinazohusu ustawi wa sekta ya kilimo nchini.
- Kuratibu na kuendesha mashirikiano katika ngazi ya taifa na wilaya
- Kuratibu jitihada za sekta ya umma na binafsi katika uenddelezaji wa kilimo-biashara

## Hii Ndiyo PFS

Ubia wa mradi wa PFS unaratibu na kuwezesha watendaji mbalimbali kwenye mnyororo wa thamani wa wadau chini ya mfumo wa mashirikiano kati ya sekta ya Umma na Binafsi (PPP). Mradi unatekelezwa na Baraza la Kilimo Tanzania. Lengo lake ni kuchangia na kuongeza kiwango cha mafanikio yaliyopatikana kwenye awamu ya pili ya Mradi wa Ubia wa Kilimo Tanzania (TAP2) katika kipindi cha Oktoba 2014 hadi Mei 2020. Mradi huo ulifanikiwa ukuaji wa kilimo kwa kutumia mbinu za kilimo-biashara na uwekezaji.

### MalengoyaMradi

**Lengo kuu ni;** Kuongeza usalama wa chakula na lishe, nakupunguza umasikini. Umaskini unatarajiwa kupungua kwa 17%, halikadhalika na ukosefu walishe kwa Watoto kupungua kwa 5%.

### Utaratibu wa utekelezaji

Mradi utatumia mbinu ya ubia katika utekelezaji wa mradi. Mradi wa PFS, chini ya Baraza la kilimo Tanzania (ACT). Utaratibu na kuongeza uwezeshaji na utekelezaji ili kuhakikisha ubia unahimarishwa na mafanikio tarajiwa yanafanikiwa. Mradi unatumia ujuzi na maarifa ili kutatua vikwazo muhimu kwenye mnyororo wa thamani. Mradi umeainisha asasi za kiraia 35, wabia kutoka sekta ya umma na binafsi (ndani na nje ya nchi), wenye uwezo na majukumu mbalimbali watakaoshirikishwa katika kazi ya ubia.

## *Bodi ya Uhariri*

1. ***Bw. Timoth Mmbaga - Mwenyekiti***
2. ***Bw. Mark Magila - Mjumbe***
3. ***Bibi. Laetitia William - Mjumbe***
4. ***Bw. Khalid Ngassa - Mjumbe***
5. ***Bibi. Susan Masagasi - Mjumbe***

## Wasiliana Na.

Mkurugenzi Mtendaji
Agricultural Council of Tanzania
S.L.P 14130, Dar es Salaam.

**Simu:** (+255) 719260726

**Barua pepe:** act@actanzania.or.tz

**Tovuti:** www.actanzania.or.tz

**Akaunti za Mitandao ya Kijamii:**

LinkedIn @barazalakilimo

Twitter @act_tz

Instagram barazalakilimotanzania

Facebook Agricultural Council of Tanzania

***PFS inawajibika kwa Bodi ya Wakurugenziwa ACT***